**Learning by Ear - Illiteracy**

**“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 04:** “**Adui wa jamii**”

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor**: Yann Durand

**Translator**: Anne Thomas

**Characters:**

**Papa Wali** *(Baba wa watoto watatu, mwenye umri wa miaka 52 – Mtoto wake wa kwanza wa kiume anaitwa Elinam, kisha anafuatwa na binti aitwaye Latifa na mwisho mtoto wa kiume aitwaye Jaurès. Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara inamwendea vibaya kila kukicha kwa kuwa hajamudu kujifunza mbinu mpya za ufundi hivi kwamba hamudu ushindani mpya wa kibiashara.)*

**Epiphane** *(Mvulana wa umri wa miaka 18, ameajiriwa na Papa Wali. Ni mwerevu sana lakini hawezi kusoma wala kuandika kwa kuwa hakupata fursa ya kujiunga na shule. Kadiri anavyopata shida kutoka na hali yake hiyo ya kutojua kusoma, ndivyo hamu yake ya kujua kusoma na kuandika inavyozidi.)*

**Zakia** *(Ana umri wa miaka 20, ni msichana aliye na uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki yake Latifa na ameajiriwa katika afisi ya wakala wa Utalii kutokana na tajriba yake ya kimasomo. Ni msichana aliyebahatika kutembelea mahali pengi na hukutana na watu wengi kazini mwake.)*

**Mr. Hendrik** *(Ana umri wa miaka 67, mtalii wa kizungu aliyestaafu na anayesafiri pamoja na mke wake Susanna.)*

**Mrs Hendrik** *(Ana umri wa miaka 62 na ni raia wa kizungu aliyestaafu na ameolewa na Bw. Hendrik)*

**Mamoua** *(Mwenye umri wa 39, mke na mama ya watoto wa Papa Wali. Ni mjamzito wa mtoto wao wa nne. Hajui kusoma na kuandika. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.)*

**Agency head** *(Mwanamke mwenye umri wa miaka 32,ndiye anayesimamia mikopo kwenye benki ya mji ya kutoa mikopo kwa biashara ndogo. Mama huyo ni mkali.)*

**INTRO:**

**Hamjambo na karibuni kwenye sehemu ya nne ya mfululizo mpya wa vipindi vya Noa Bongo-Jenga , Maisha yako ya "Msichana ahitimu"; makala inayohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Ingawa Zakia ni msichana huru anayejikimu maishani, kwa kawaida hayaingilii moja kwa moja masuala ya elimu ya Latifa. Hata hivyo wazazi wa Latifa wanashuku kwamba huenda Zakia ndiye mshauri wake.Kutokana na hali hiyo, mamake Latifa, Mamoua ameondokea kumchukia Zakia na kila mara anamsema vibaya.*

*Asubuhi hiyo hakuna aliyetarajia Zakia atapitia kwenye karakana ya Papa Wali akiandamana na Watalii wa Kizungu, Bwana na Bibi Hendrik. Sikiliza sehemu ya nne:* ***Adui wa jamii.***

## Scene 1, IN PAPA WALI’S WORKSHOP

Papa Wali, Epiphane, Zakia, Bwana na Bibi Hendrik

1. **SFX ATMO: METAL SAW + HAMMERING ON A METAL SHEET / FOOTSTEPS APPROACHING (3 PEOPLE)**

2. **Papa Wali:** Karibuni!

3. **Zakia:** Asante mjomba!

4. **Mr Hendrik:** Asante!

5. **Mrs Hendrik:** Hujambo!

6. **Papa Wali:** (**Jovially**) Hamjambo. Habari zenu?

7. **Mr Hendrik:** Hatujambo hatujui wewe?

8. **Papa Wali:** Nasi pia hatujambo!

9. **Zakia:** Mjomba, huyu ni Bwana Hendrik na mke wake. Ni watalii. Wangetaka kutizama karakana yako.

10. **Papa Wali:** Ukweli? Haya basi!

11. **Zakia:** (**To the couple**) Papa Wali ndiye mwenye karakana hii.

12. **Mr & Mrs Hendrik:** Tumefurahi kujuana nawe, Papa Wali!

13. **Papa Wali:** Mimi pia. (**To Zakia**) Nadhani ninakufahamu, lakini...

14. **Zakia:** Jina langu ni Zakia. Mimi ni rafiki yake Latifa.

15. **Papa Wali:** Naam. Unafanya kazi inayohusu watalii. Latifa aliwahi kunidokezea...

**16. Zakia:** Naam, katika ofisi ya wakala wa safari za watalii.

**17. Papa Wali:** Vizuri! Na hawa wageni wetu wanatafuta?

**18. Zakia:** Wanataka kuona jinsi unavyofua na kuchomelea vyuma.

**19. Papa Wali:** Haya basi! Karibuni mkae!

**20. Mr & Mrs Hendrik:** Asante!

**21. Papa Wali:** Epiphane!

**22. Epiphane:** Mzee?

**23. Papa Wali:** Huoni kwamba tumepata wageni? Waletee viti na maji safi badala ya kukaa kuwatizama kama kwamba ni viumbe kutoka mwezini. Kwani hujawahi kuona wazungu maishani mwako?

**24. Epiphane:** La… Naam mzee! (**He runs into the workshop**)

**25. SFX ATMO: QUICK FOOTSTEPS. LOUD CRASHING NOISES + CHAIRS BEING PUT DOWN**

**26. Mr Hendrik:** Naomba nimsaidie; hapana wasiwasi…

**27. Papa Wali:** La, la, hasha. Hahitaji usaidizi. Mara nyingi yuko hapa bila la kufanya. (**Silence. To Epiphane**) Umevipangusa vizuri hivyo viti?

**28.** SFX ATMO: CARRYING CHAIRS, POURING WATER INTO GLASSES

**29. Epiphane:** Ndiyo, mzee!

**30. Mr Hendrik:** Usijisumbue sana kwa ajili yetu. Hatuna neno. **(Silence**) Hapa unafanya nini?

**31. Papa Wali:** (**Proudly**) Oh, hapa? Ninatengeneza kipande cha samani ya sebuleni kwa kutumia vyuma.

**32. SFX ATMO: METAL SAW + HAMMERING ON A METAL SHEET**

**33. Mrs Hendrik:** Kwani kuna mtu ameagiza bidhaa hii?

**34. Papa Wali:** Hapana, ni sampuli ya maonyesho. Mteja yeyote atakayeihitaji anawezakuinunua.

**35. Mr Hendrik:** Inapendeza si haba!

**36. Mrs Hendrik:** Tunaweza tukutazame unavyofanya kazi yako?

**37. Papa Wali:** Bila shaka! Hilo si tatizo!

**38. SFX ATMO : NOISE OF ARC WELDING**

**NARRATOR:** *Watalii wanaposhuhudia shughuli za Papa Wali kwenye karakana yake, Mamoua naye yuko upande mwingine wa mji akikabiliana na mkuu wa taasisi ya fedha inayofadhili biashara ndogo iliyompa mkopo.*

**Scene 2, AT THE MICRO-FINANCE AGENCY**

Mamoua na mkuu wa taasisi ya kifedha

**39. SFX ATMO: OFFICE SOUNDS – UNCLEAR VOICES - PRINTER – PHONES RINGING**

**40. Agency head:** Mama Mamoua, Tulikukopesha fedha ili uimarishe biashara yako wala si kwenda kumzika mama yako!

**41. Mamoua:** Kwa hivyo nikifikwa na mkosi na nina fedha, sifai kuzitumia?

**42. Agency head:** Hapana! Hizo fedha si za matumizi yako! Fedha hizo zimenuiwa kuiimarisha biashara yako!

**43. Mamoua:** Mama, ni muhimu nimzike mamangu kwa heshima inayohitajika kwani ni tukio la mara moja tu maishani. Hata hivyo nitawalipa fedha zenu hivi karibuni.

**44. Agency head:** Hivi karibuni? Inaoenekana huelewi athari za maamuzi yako. Kamwe huwezi kutumia vibaya pesa ulizokopeshwa na benki! (**Shouting**) Tabia gani hii ya kutojua kusoma?

**45. Mamoua:** Kwanini unanitusi? Nimesema nitawalipa fedha zenu!

**46. Agency head:** Hujalipa chochote tangu miezi mitatu iliyopita, mama. Biashara yako haiongezeki na inaelekea kuzorota kila kukicha!

**47. Mamoua:** Mume wangu sasa hivi anakabiliwa na matatizo. Biashara yangu ndogo ndiyo inayoilisha familia nzima. Mara nyingine inanibidi nimkopeshe fedha ili alipe gharama ya nguvu za umeme kwenye karakana yake.

**48. Agency head:** Alaa! Kwa hivyo wewe ndiye mhisani na mimi mkopeshaji ndiye mbaya. Si mumeo pekee anayehitaji fedha. Sisi pia tunahitaji fedha hasa ukizingatia kuwa fedha unazozizungumzia zimetoka kwetu sisi! (**Scornfully**) Hebu ondoka! Nenda zako tafadhali!

**49. Mamoua:** Asante sana, mama!

**50. SFX ATMO:** **CHAIR+ STEPS GOING AWAY**

**51. Agency head:** (**Alone**); Mwanamke wa ajabu huyo! Watu ambao hawajasoma ndio wasiozingatia mambo kama huyo mama alivyo!

**NARRATOR:** *Mama Mamoua alisumbuka roho alipogundua jinsi watu wa kawaida wanavyoonewa... Lakini ebu turejee kwenye karakana ya Papa Wali. Anajivunia karakana yake. Ingawa anakabiliwa na hali ngumu, amepata fursa ya kuwaonyesha watalii wa Kizungu ujuzi wake.*

## Scene 3, IN PAPA WALI'S WORKSHOP

Papa Wali, Epiphane, Zakia, Bw. na Bi. Hendrik

**52. SFX ATMO: NOISE OF ARC WELDING + HAMMERING ON A METAL SHEET**

**53. Mr Hendrik:** (**He shouts over the noise**) Kwani huna vifaa vya kujikinga na cheche?

**54. Papa Wali:** Wasemaje? **(interrupting his work)**

**55. Mr Hendrik:** Mbona huvai glavu au kofia ya kujikinga kutokana na cheche na miale?

**56. Papa Wali:** Mbona sikuelewi?

**57. Mr Hendrik:** Wajua, ndimi za moto wa mashine ya kuchomelea ni hatari sana. Zina miale ambayo inaweza kuharibu mtoto wa jicho na kuingilia zaidi viungo vya ndani. Inakubidi uvae kofia ya kujikinga, glavu na magwanda ya kujikinga yaliyotengenezwa kwa ngozi ya mnyama. Miale hiyo haipenyi ngozi ya mnyama iliyokaushwa.

**58. Papa Wali:** Lau ningekuwa na fedha za kufanya yote hayo, ningezitumia fedha hizo kugharamia vitu tunavyohitaji nyumbani! Nimekuwa nikifanya kazi zangu hivi hivi! Sijawahi kuugua macho. Nyinyi watu wa mataifa ya magharibi hali zenu dhaifu. Si sisi!

**59. Zakia:** Papa Wali, hivyo ndivyo tunavyodai kila wakati, na tunapoangamia bila sababu tunasema kwamba ni kwasababu ya uchawi!

**60. Papa Wali:** Zakia, mbona nyie vijana wa leo mnajipa kufahamu mengi ya dunia kuliko wazee wenu?

**61. Mrs Hendrik:** Hatujanuia kukukosea heshima, Papa Wali! Wasiwasi wetu ni afya yako tu ukizingatia athari zilizopo. Sote hapa tumo hatarini. Hata hivyo umesema kweli. Mazoea yanampa mtu uzoefu mwingi!

**62. Mr Hendrik:** (**Looks at Epiphane working**) Huyu kijana anafanya nini?

**63. Papa Wali:** Epiphane? Anakunja vyuma vya kutegeneza viti.

**64. Mr Hendrik:** Bila shaka ni kazi ngumu kuhakikisha kuwa vyuma vyote hivi vina umbo sawa...

**65. Papa Wali:** Tumeshazoea! Epiphane amefunzwa akafunzika!

**66. Mr Hendrik:** Huoni kama kwamba utafaidika ukizipa kandarasi kampuni zenye vifaa vinavyofaa kwa kazi yako hii?

**67. Papa Wali:** Una maana gani?

**68. Mrs Hendrik:** Uzilipe fedha kampuni hizo ili zikukunjie vyuma vyako.

**69. Mr Hendrik:** Hivyo utatumia muda mfupi bila kuchoka sana. Utakuwa na hakika ya kupata vyuma vyenye umbo sawa.

**70. Papa Wali:** Nimesikia kwamba karakana ya vyuma iliyo karibu na soko ina mashine kubwa. Lakini bila shaka bei yao ni ghali!

**71. Zakia:** Tumeshakwenda huko pia.

**72. Mr Hendrik:** Wapi? Mahali tulipokuwa hapo kabla?

**73. Zakia:** Naam…

**74. M. Hendrik:** Kama uko radhi, tutakupitia hapa kesho tuandamane hadi huko. Hutopoteza chochote kwenda kujulia hali ya mambo huko.

**75. Zakia:** Je mjomba umekubali?

**76. Papa Wali:** Sawa, njooni wakati wowote hapo kesho. Nitawasubiri hapa.

**77. Mrs Hendrik:** Huyu Epiphane ni mwanao au mfanyikazi wako?

**78. Papa Wali:** Epiphane ni mfanyikazi wangu.

**79. Mrs Hendrik:** Amejifunzia wapi kazi hii?

**80. Papa Wali:** Hapa hapa! Alikuwa mwanafunzi wangu. Sasa hivi ni mfanyikazi mzuri.

**81. Mrs Hendrik:** Kwa hivyo, unamlipa mshahara?

**82. Papa Wali:** Eee… Hapana… Wajua sikumdai karo nilipokuwa nikimfunza kazi. Hivi analipia mafunzo aliyopata kwa kunifanyia kazi. Yeye hulala hapa na kula hapa...

**83. Mrs Hendrik** Analala katika karakana? Kwani hana jamaa?

**84. Papa Wali:** Hapana, yeye ni yatima. Alikuwa akiishi barabarani kabla ya kujiunga nami. Hajaondoka hapa tangu nilipompokea !

**85. Mrs Hendrik:** Je alihudhuria shule?

**86. Papa Wali:** Hapana!

**87. Mrs Hendrik:** Ukweli? (**To Epiphane**) Epiphane, uko sawa?

**88. Epiphane:** (**Stops hammering**) Ndiyo, mama!

**89. Mrs Hendrik:** Kwani hukutaka kujua kusoma na kuandika?

**90. Epiphane:** Nilitaka, mama!

**91. Mrs Hendrik:** (**to Papa Wali**) Waonaje akianza kusoma jioni jioni?

**92. Papa Wali:** Kwangu ni sawa! Lakini sijui hilo litamsaidia vipi!

**93. Mr Hendrik:** Litamsaidia bila shaka. Kuandika risiti, kutayarisha maagizo ya wateja, kuandaa vipimo, kuandika jina, kuandaa mahesabu, kufahamu haki za mfanyikazi, kutangaza bidhaa za karakana... Mtu anaweza kufanya mengi kwasababu ya kusoma masomo.
(**Laughing**) Na wewe pia unaweza kuhudhuria masomo ya jioni! Mbona usianze? Utajiimarisha zaidi kikazi.

**94. Papa Wali:** Ebu nifikirie mimi nikiwa nimekalia mabao shuleni pamoja na watoto! Aibu!

**95. Mr Hendrik:** Papa Wali, wala si aibu kujua kusoma na kuandika na kuwa na uwezo wa kumwandikia mteja orodha ya vitu anavyokulipa. Madarasa ya joini yamepangwa kutegemea umri na ufahamu wako.

**96. Mrs Hendrik:** Mpe muda afikirie hayo, Charles.

**97. Mr Hendrik:** Bila shaka! Hata hivyo, hongera! Unapenda kazi yao si haba! Huo ni mwenendo mzuri!

**98. Mrs Hendrik:** Tunaweza kununua samani kutoka kwako?

**99. Papa Wali:** Bila shaka!

**100. Mrs Hendrik:** Sawa! Tutakuja kununua kabla hatujaondoka. Tunakushukuru kwa wema wako! Mimi na mume wangu tuna wakfu tunaouita Wakfu wa Hendrik. Tunalenga kuzisaidia biashara ndogo ndogo barani kuongeza ujuzi na utendakazi, hasa kupitia mafunzo na ushauri. Tutazungumza zaidi kesho. Sawa?

**101. Papa Wali:** Sawa! Asanteni kwa kunitembelea!

**102. Mrs Hendrik:** Si neno, Papa Wali! Kwaheri!

**103. SFX ATMO: SOUND OF CHAIRS AND STEPS**

**104. Mr Hendrik:** Kwaheri na asante sana!

**105. Papa Wali:** Kwaheri! Tutaonana kesho!

**106. Mrs Hendrik:** Tutaonana kesho, Epiphane!

**107. Epiphane:** Naam, tutaonana kesho!

**108. Mr Hendrik and Zakia:** Tunaonana kesho!

**OUTRO:**

*Kutojua kusoma na kuandika ni hali ambayo huenda ikawa kikwazo cha mawasiliano, uhusiano mzuri wa kijamii, na pia maendeleo. Je Papa Wali na familia yake wataweza kuutua mzigo huo? Je Wakfu wa Hendrik utamsaidia vipi? Upi mustakabla wa Latifa? Je maisha yake ya kila siku nauhusiano na wazaziwake utaimarika? Je ataweza kupata nafasi yakuthibitihsa kuwa mtazamowawazazi wake ulikuwa si sahihi?Kwa mengi zaidi sikiliza kipindi kifuatacho cha "**Msichana ahitimu**", mchezo wa redio kuhusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.*

**Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au vyengine vya mfululizo wa Noa Bongo-Jenga Maisha yako tazama ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe. Anuani ni:** lbe@dw-world.de

**Shukran kwa kuwa nasi. Hadi wakati mwingine nakutakia kila la kheri!**

**END OF 4th EPISODE**